# Sign Industries ni nini na Inafanya kazi gani?


Bango ndilyo kitu cha kwanza na moja ya nafasi nzuri kabisa za kufanya mawasiliano na wateja na umma kwa ujumla. Mabango yanapaswa kusanifiwa vizuri, kutengenzwa vizuri na kusimikwa vizuri, kuwekwa na kuoneshwa kwa namna inayotoa ujumbe kwa ubora zaidi.

Kwa mtizamo wa kibiashara, bango halichukuliwa kama hasara bali kama uwekezaji. Linatengenezwa na kugharamiwa mara moja lakini kwa matunzo sahihi, litadumu kwa miaka na kurejesha mtaji kwa maelfu.

Kwa kuzingatia mtizamo huu wa uwekezaji, Sign Industries ni wabobezi wa kukidhi mahitaji ya mteja na kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma zetu zinakidhi imani ya uwekezaji ya wateja wetu, tumedhamiria kutoa bidhaa na huduma bora tu.

## Kwa hiyo tunafanya nini hasa?

Tuna huduma sita za msingi katika utendaji kazi wetu.
1] Ushauri wa kitaalamu
2] Usanifu - kutoka wazo hadi kitu kinachoonekana
3] Kupata vibali kutoka mamlaka za manispaa
4] Kuuza bidhaa zinahusiana na mabango.
5] Usimikaji
6] Ukarabati na huduma baada ya mauzo.




## 1] Ushauri wa kitaalamu

Sign Industries Ltd. tunatoa huduma ya ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya mabango ya ujenzi na mengineyo ya kawaida.

### Ushauri kabla ya ujenzi:

Tunapendelea kushirikishwa tangu hatua za mwanzo za mradi au wakati wazo linabuniwa kabla hata ujenzi haujaanza. Kwa jinsi hiyo, tunaweza kushirikiana na wasanifu majengo ili kutenga maeneo kwa ukubwa wa mabango, kuonekana, kufikiwa, urefu na eneo la mvuto wa bango litakaposimikwa hapo baadae.

### Ushauri baada ya ujenzi:

'Kamwe hakuna kuchelewa', na hiyo ndiyo kauli mbiu yetu. Ama kutokana na kusahau, mipango mibaya, kutokuwa na fedha za kutosha au mabadiliko ya uongozi au kutokana na sababu nyingine nyingi, baadhi ya majengo au ujenzi hauna mabango yoyote au kuna upungufu wa mabango. Katika hali hiyo, tunatoa mapendekezo kamili na mipango ya kuweka mabango ndani na nje ya maeneo hayo na mpango kamili wa mfumo wa mabango. Kipaumbele chetu kikubwa wakati wote ni kuangalia uwezo wa kifedha wa mteja.

## Nini kinachozingatiwa katika ushauri wa kitaalamu?

Tunatembelea eneo (wakati mwingine zaidi ya mara moja) na kuchukua vipimo vyote na picha. Michoro ya usanifu inalinganishwa na umbo ambalo linawekwa kwa utaalamu wa hali ya juu (super imposed) kupata taswira ijulikanayo kama 'WYSIWYG ', (what you see is what you get) yaani, “unachokiona ndicho utakachokipata”. Usanifu wote unafanyika kwa kipimo na uwiano sahihi, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo. Kwa njia hii, mteja na kampuni yake ya usanifu wataweza kupata picha halisi ya kinachotarajiwa.

Ushauri wa kitaalamu unahusisha na mambo yafuatayo;
1] Kwa nini ninahitaji bango?
2] Wakati gani ninahitaji bango?
3] Wapi niweke bango langu?
4] Nani ana sifa ya kuwa mtengeneza mabango yangu ?
5] Aina gani ya bango ninalohitaji?
6] Aina gani ya umbo ninalohitaji kwa bango langu?
7] Namna ya kupata mwonekano wa gharama bila ya kutumia fedha zaidi.
8] Mambo ya kufanya na kutofanya kuhusiana na bango.

Mara nyingi,  timu ya ushauri inaundwa na mshauri wetu, timu ya wafanyakazi kutoka idara ya matengenezo na usimikaji, wasanifu michoro, mafundi umeme na waashi na mafundi wengine, wengi wao kutoka katika kampuni yetu.

## 2] Michoro ya Kisanifu

Mabango yanatafsiriwa kama ‘Lugha ya Mawasiliano kwa Macho’ wakati Michoro ya Kisanifu inatafsiriwa kama ‘Sanaa ya mawasiliano kwa macho.’ Mambo hayo yanasaidiana na zao la mwisho. Mchoro wa kisanifu unapaswa kumsisimua mlaji ili kubadilisha tabia yake ya kufanya manunuzi. Lakini siyo kila mara yanamlenga mteja. Wakati mwingine, ni kwa ajili ya kuonesha ueleko au kutoa maelezo, ya lazima, ya makatazo au alama za usalama na mambo kama hayo. Kwa hiyo ni muhimu kuainisha madhumuni na kutengeneza umbo zuri na la kupendeza, ujumbe, alama au ubunifu kwa ajili ya madhumuni ya bango.

Baada ya kuingia kwa teknolojia ya uchapaji wa kidijitali kwa ujumla, mchoro wa kisanifu ulio mbaya utakuwa umetenda makosa makubwa sana kwa uwezo wa teknolojia ya kisasa. Idara yetu ya Sanaa itaendelea wazo kulingana na bango lenyewe, walengwa na utamaduni wa eneo ambako jambo linatakwa kufanyiwa promesheni.Tunao uwezo wa kutosha wa vifaa na programu za kompyuta na rasilimali watu wa kubuni michoro ya kisanifu ambayo ama inaweza kupigwa chapa au kutengeneza bango. Wakati mwingine tunafanya kazi na wakala wa mabango na kuwaongoza kufikia kupata kitu kizuri.

## Aina za Mabango:

Kuna aina nyingi za mabango lakini yanayoainisha mara nying ni ya ndani na ya nje

## 3] Kuwasiliana na mamlaka za manispaa

Inatubidi kukiri kwamba hili ni eneo moja ambalo tusingependa kujihusisha nalo. Hilo hasa linatokana na ukiritimba katika ofisi za Halmashauri ya Jiji. Hakuna sheria hata moja au shera ndogo inayohusu eneo hili ambayo haina utata na jambo hili limezua wasiwasi mkubwa kwa jamii ambayo pia inalalamikia kodi kubwa inayotozwa kwa mabango makubwa. Kukosekana kwa ushirikiano kati ya ofisi za Halmashauri ya Jiji na TANROADS, wenye dhamana kuhusu matengenezo ya barabara , kumechangia kwenye mkanganyiko huu kutokana na ukosefu wa mawasiliano katika ya mamlaka hizo mbili. Hata hivyo, hatupendi kushughulika na sehemu hii, wakati mwingine tunalazimika kumfanyia kazi mteja nje ya imani yetu kama sehemu ya “Huduma yetu Kuongeza Thamani ya Fedha.” Maelezo zaidi yanapatikana kwenye tovuti yetu kiungo cha “Sheria za Jiji” (Bado inatengenezwa).

## 4) Tunasambaza nini?

Kazi nyingi za masanduku ya kutoa nuru, mabango yanayotoa nuru na yasiyotoa nuru, mabango ya nguzo kubwa, mabango ya ‘Neon’, na vifaa vya POP (Point of Purchase na POS (Poin tof Sale) zimetengenezwa nasi. Baadhi ya malighafi na bidhaa zilizokamilika pia tunaagiza kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, mabango ya mduara ya kuonesha mwelekeo yatengenezwayo kwa kutumia maumbo ya aluminium iliyoimarishwa yanaagizwa kama malighafi kutoka kiwandani kisha kutengenezwa katika bango la kuonesha uelekeo au aina ya bango linalotakiwa. Vifaa vya mabango ya ‘Neon’, mabapa ya akriliki, nailoni maalum aina ya ‘flex’ na vitu vingine vya POP na POS pia vinaagizwa kutoka nje  na kisha kukamilishwa nasi. Masanduku yetu ya mabango  tunayotengezana mabango ya kutoa nuru ni kulingana na viwango vya kimataifa na tunatumia tu vifaa vya umeme vilivyoidhinishwa na UL. (Underwriter Laboratories).   Utengenezaji masanduku na uimarishaji wake unafanyika kwa kutumia chuma kisichopata kutu na hali inayoweza kuchangia kupunguza ubora wake na uchakavu utokanao na hali ya mazingira.

## 5) Usimikaji


Hii ni sehemu kubwa ya huduma yetu na tunawashauri sana wateja wetu kutojaribu kufanya kazi ya usimikaji wa mabango na kuchukua jukumu wao wenyewe ili kuokoa fedha. Waranti yetu pia itabatilika iwapo tangazo litasimikwa na watu wengine. Sisi tumesajiliwa na kuidhinishwa na bodi ya wajenzi na pia tumekata bima zote muhimu na tunaajiri watu wenye weledi na uzoefu mwingi na kutumia vifa sahihi kwa kazi hiyo. Tunasimika mabango yote tunayotengeza au kusambaza. Mara chache tunafanya kazi kama makandarasi wa kando ili

kusimika mabango yaliyotengezwa na wengine. Tumesimika mabango kwenye mapaa ya nyumba, barabara kuu na kando ya barabara, kwenye maeneo ya shughuli na yasiyokuwa ya shughuli na pia kwenye maeneo yasiyokuwa ya kawaida. Mabango yetu katika ukubwa na maumbo mbali mbali yamesimikwa nchi nzima.

## 6) Ukarabati na huduma

Tunatoa waranti kwenye mabango yetu yote ye LED na bidhaa nyingine inayotengenezwa au kusambazwa nasi. Hata hivyo, inashauriwa kuingia mkataba wa huduma ili kuongeza waranti ili kuwa na bango lisilokutia wasi-wasi na hilo linatekelezwa bila masharti. Licha ya hivyo, bidhaa yoyote inayotengezwa au kusambazwa nasi tunaihudumia mara moja endapo kutakuwa na kutofanya kazi kokote au hata kama mteja atahitaji mabadiliko yoyote yanayoweza kutokea baadae.  Kutokana na ubora wa vifaa tunavyotumia katika utengenezaji wetu, kupigiwa simu ya kufanya matengenezo ni jambo la nadra sana kutokea.

## Usimikaji wa kitaalamu (Professional Installation)



*Bango la "flexy" la futi za mraba 160 likisimikwa kwenye ghorafa ya  tisa kwa kutunia kreni yenye mkono mrefu.*



*Bango la nguzo kubwa la ukubwa wa 7mx2mx0.6m likisimikwa kwenye kitako cha zege ambacho pia kimetengenezwa nasi.*





*Bango la 6mx3m likisimikwa kwenye kitako cha zege ambacho pia kimetengezwa nasi.*

## Mabango yakiwa tayari kwa kusafirishwa nje ya nchi

